

Maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika - wakati matibabu hayatolewi

Taarifa kwa mgonjwa kutoka kwa daktari wa magonjwa ya kuambukiza nchini Uswidi.

Kwa nini nimepokea taarifa hii?

Kipimo kimeonyesha kwamba una maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika.

Hapa kuna taarifa ya mambo ya kuzingatia.

Maambukizi yaliyofichika ya kifua kikuu ni nini?

Maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika yanamaanisha kwamba umeambukizwa bakteria za kifua kikuu, lakini huna ugonjwa kutokana nayo. Mtu anapoambukizwa bakteria za kifua kikuu, mfumo wa kinga ya mwili huitikia na hii inaweza kupimwa kwa kipimo cha damu au kipimo cha ngozi. Watu wengi walioambukizwa huendelea kuwa na afya njema, lakini kuna hatari ndogo ya kuugua kifua kikuu baadaye maishani.

Je, maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika yanaambukiza?

Hapana, maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika hayaambukizi. Kifua kikuu kinaweza kuambukiza tu wakati mtu ni mgonjwa na ugonjwa wa kifua kikuu uko kwenye mapafu.

Je, kuna matibabu ya maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika?

Watu walio katika hatari kubwa ya kuugua kifua kikuu hupewa matibabu ya kuzuia. Hii inatumika, kwa mfano, kwa watoto na watu walio na kinga dhaifu.

Daktari wako ameamua kwamba **huhitaji** matibabu sasa.

Ninapaswa kuzingatia nini?

Ikiwa katika siku zijazo utapata dalili za muda mrefu (zaidi ya wiki tatu) kama vile kikohozi, homa, kutokwa na jasho usiku au kupungua uzito bila kukusudia, unapaswa kuwasiliana na daktari. Mwambie kwamba una maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika.

Ukipata mimba au kupata kisukari kinachotibiwa kwa insulini, ugonjwa mbaya wa figo, matibabu ya saratani, au kinga dhaifu kwa sababu nyingine, unapaswa kumwambia daktari wako kwamba una maambukizi ya kifua kikuu yaliyofichika. Huenda ukahitaji matibabu ya kinga ili kuepuka kuugua kifua kikuu.

Taarifa ya mawasiliano (Kontaktuppgifter)

Kitengo cha matibabu (Mottagning).....

.....

Simu (Telefon).....